

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**



**TANGAZO LA KUITWA KAZINI**

Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) inapenda kuwataarifu waombaji wote wa kazi za mkataba katika programu ya Mpango wa Uwekezaji katika Afya ya Mama na Mtoto nchini Tanzania (Tanzania Maternal and Child Health Investment Program (TMCHIP) waliowasilisha maombi ya ajira kwa nafasi mbalimbali za kada za afya katika kipindi cha mwezi wa Desemba, 2024 kuwa mchakato wa kuwapangia vituo vya kazi umekamilika hivyo waombaji wote waliochaguliwa wanatakiwa kuripoti katika Halmashauri walizopangiwa.

Waombaji wote walio pata nafasi wanatakiwa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

- i) Kuripoti katika vituo vya kazi walivyopangiwa katika muda wa siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili. Aidha, waombaji watakaoshindwa kuripoti kwenye vituo vya kazi ndani ya siku kumi na nne (14) nafasi zao zitajazwa na waombaji wengine haraka iwezekanavyo;
- ii) Kuwasilisha Vyeti Halisi (**Original Certificates**) vya Kidato cha Nne, Sita, Chuo Kikuu, NACTE na vyeti halisi vya usajili wa mabaraza ya kitaaluma kwa ajili ya kuhakikiwa na mwajiri kabla ya kupewa barua ya ajira;
- iii) Waombaji waliopata nafasi za ajira watakaoripoti bila ya kuwa na Vyeti Halisi (**Original Certificates**) vya Kidato cha Nne, Kidato Sita, Chuo Kikuu, NACTE na vyeti halisi vya usajili wa mabaraza ya kitaaluma hawatapokelewa;

iv) Waombaji waliopata nafasi za ajira wanajulishwa kuwa hakutakuwa na nafasi ya kubadilisha vituo vya kazi walivyopangiwa.

Waombaji wote ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili, watambue kuwa hawakupata nafasi hivyo wasisite kuomba kwa mara nyingine nafasi za kazi zitakapotangazwa.

Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaelekezwa kuwapokea, kuhakiki vyeti na kuwafanyia mafunzo elekezi (Induction Course) kabla ya kuwapangia vituo vya kazi.

Orodha ya majina ya waombaji waliopangiwa vituo vya kazi inapatikana kupitia tovuti ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI [www.tamisemi.go.tz](http://www.tamisemi.go.tz)

**Limetolewa na:**

Katibu Mkuu,  
Ofisi ya Rais - TAMISEMI,  
Mji wa Serikali – Mtumba,  
S.L.P. 1923,  
**DODOMA.**

**15 Machi, 2025**









<b>Na.</b>	<b>Jina la Muombaji</b>	<b>Jinsi</b>	<b>Kada</b>	<b>Mkoa</b>	<b>Halmashauri</b>	<b>Kituo</b>	<b>Namba ya Maombi</b>	<b>Mwaka Kuhitimu Chuo</b>
435	ANITHA BENEZETH JOHN	FEMALE	Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II	Tabora	Tabora Municipal Council	IKOMWA	0005120-1224	2019